


JIMBO KATOLIKI LA SUMBAWANGA

CHUO CHA KILIMO LAELA

E-mail: laelalac@yahoo.com



P.O.BOX 21, LAELA , RUKWA

Kilimo endelevu ni chaguo letu

NAMBA YA USAJILI: REG/NACTVET0654

1.0 Historia ya chuo

Kituo cha kilimo Laella kilianzishwa mwezi Septemba 1990 kama mradi chini ya jimbo katoliki la Sumbawanga. Mradi huu ulikuwa ni matokeo ya majadiliano kati ya mamlaka za jimbo, Parokia ya Laelana wadau wa maendeleo nchini Uholanzi. Majadiliano haya yaliongozwa na Paroko wa Parokia ya Laela wakati huo Fr. Piet van de pas (Simchile)

Mradi ulikuwa umekusudiwa kutekelezwa katika awamu mbili, awamu ya kwanza ya matazamio (pilot phase) kati ya mwaka September 1990 hadi August 1995. Awamu ya pili ya utendaji (operational phase) kuanzia September 1995 hadi August 1998. Katika tathimini iliyofanyika mwaka 1995, ilionekana kwamba mradi huu umefika mahali ambapo ni lazima iwekwe mikakati ya kuundeleza zaidi ili uweze kutoa huduma zaidi ya ilivyo fikiriwa awali kwa kuwa uhitaji kwa walengwa ulikuwa ni mkubwa.

2.0 Maono na utume wa Kituo

2.1 Maono

Jamii inayoishi maisha mazuri na inapata mahitaji ya msingi. Jamii inayoamini katika haki za binadamu na inaishi katika mazingira mazuri

2.2 Utume

Kituo kinatoa elimu, shughuli za ugani, ufikio wa masoko na huduma nyingine kwa wakulima wadogo kikilenga kukuza kilimo endelevu. Kituo pia kina hamasisha ushirikiano kupitia vikundi, kuhamasisha maswala ya jinsia na utunzaji mazingira. Kituo pia kinajitahidi kujiimarisha ili kiweze kuwa taasisi imara ilioendelevu kitaasisi na kiuchumi.

3.0 Shughuli za Kituo

3.1 Mafunzo

3.1.1 Mafunzo ya muda mrefu

Kituo cha Kilimo Laela kimekuwa kikitoa mafunzo ya muda mrefu ya mwaka mmoja kwa vijana tangu kilipoanzishwa. Walengwa wa mafunzo haya walikuwa ni vijana waliohitimu darasa la saba na kuendelea. Lengo la mafunzo haya lilikuwa kuwapatia ujuzi vijana waliokosa nafasi za kuendelea na masomo ya sekondari, ujuzi utakao wasaidia ili waweze kujajiri kuitia kilimo na ufugaji. Kozi hii haikuwa imesajiliwa na serekali kwa hiyo cheti kilichotolewa kilikuwa ni cheti cha kawaida cha kuhitimu. Mwaka 2020 serikali ilishauri kozi hii isajiliwe ili wahitimu waweze kupata vyeti vinavyo tambulika. Mwaka 2020 mwezi Novemba usajili ulikamilika kwa kusajili chini ya VETA wakati ule.

3.1.2 Mafunzo kwa wakulima watu wazima

Kituo kinatoa mafunzo ya Kilimo na ufugaji bora kwa wakulima vijijini. Mafunzo haya yanatolewa kuitia vikundi nya wakulima.

3.2.0 Shughuli nyingine

3.2.1 Mashamba ya maonyesho/majaribio/mashamba darasa:

Kituo kinafanya majaribio ya teknoljia mpya na kufanya maonyesho kwa wakulima ambayo ni rafiki kwa mazingira. Kituo kinashirikiana na Taasisi ya utafiti ya Uyole katika kufiksha tafiti mbalimbali kwa wakulima.

3.2.2 Hifadhi ya mazingira

Kituo kinashughulika na utunzaji wa mazingira kwa kutunza miti iliyopo lakini pia kupanda miti mipy. Wanafunzi wetu wanafundishwa utunzaji wa mazingira kama sehemu ya kilimo endelevu.

4.0 Malazi

Kituo kina mabweni ya kulala kwa wanafunzi wote wa kiume na wakike. Hata hivyo tunapokea pia wanafunzi wanaoishi nje ya kituo, wote wa kike na wakiume.

Mawasiliano:

1. 0787 284 585 – Meneja
2. 0759 435 595 – Mratibu mafunzo

